

# **KAFARA YA YESU**

**DR. MUFTI MUHAMMAD SADIQ R.A.**

**JUMUIYA YA WAISLAMU WA AHMADIYYA**

## **KAFARA YA YESU**

**Mtunzi: Dr. Mufti Muhammad Sadiq r.a.**

**Mfasiri: Bwana Athumani Gakuria**

© Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya - Tanzania  
S.L.P. 376, Dar us Salaam - Simu 110743- Fax 121744

Chapa ya mara ya kwanza Kiingereza.  
Chapa ya mara ya pili 1966, 10,000  
Chapa ya mara ya tatu, 1978 5,000  
Chapa ya mara ya nne, 2000 5,000

Kimeenezwa na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya  
Tanzania

Kimechapishwa na Ahmadiyya Printing Press  
P. O. Box 367  
Dar us Salaam

# بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

*Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema,  
Mwingi wa Ukarimu.*

## DIBAJI

Kitabu ambacho nina heshima kuweka mbele yenu katika kurasa zifuatazo kiliandikwa na Marehemu Dr. Mufti Muhammad Sadiq (Mwenyezi Mungu awe radhi naye) aliyekuwa mbashiri wa kwanza kupelekwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya katika nchi ya Amerika. Kitabu hiki kilivyokuwa na hoja zenye kupenya katika nyoyo za watu kilileta badiliko sana katika nchi hiyo na maelfu ya wananchi wakajiunga na Dini ya Kiislamu ambayo ndiyo Dini ya pekee iliyoletwa ulimwenguni humu kwa ajili ya watu wote na mataifa yote. Tangu hapo wabashiri wetu wamekwenda huko kwa wingi na Jumuiya imepata nguvu katika nchi hiyo.

Ukristo unaojidai kuwa dini ya watu wote umekosa mafundisho safi na hoja zenye kueleweka akilini. Ndiyo sababu wafuasi wake wengine wanauchukia na idadi ya watu hao inazidi kukua kila siku. Nusu nzima ya Wakristo wa Ulaya na Amerika hawaupendi Ukristo wa siku hizi, bali wamebaki kama watu wasio na dini yoyote. Hata wengine wao hawamwamini Mungu. Hali hii imepatikana kwa sababu watu wa Magharibi wanataka ile dini iliyo na mafundisho yenye kukubalika akilini na inayoweza kufuatwa katika "zama hizi za elimu" ambayo inaweza kuondoa shida zao maishani na kuwaongoza katika mambo yote. Si kweli kusema kwamba watu hao hawataki dini kwa jumla, la, bali Ukristo tu umewachosha.

Hapa Afrika wananchi wengi waliupokea Ukristo kama dini ya Mzungu. Serikali za Kikristo zilitumia hila nyingi kuimarisha utawala wa kigeni. Tangu mwaka 1961, yaani baada ya uhuru kuanza kupatikana hapa Afrika ya Mashariki, wananchi wameng`amua uhusiano mkubwa baina ya Ukristo na Ukoloni na wanajitahidi kujiokoa na vyote viwili. Katika hali kama hii ninafikiri kitabu hiki kitawafaa

sana wasomaji na kuwajulisha kwa nini watu wanaichukia dini ya Kikristo.

Ninasifu kazi ya Bwana Athumani Gakuria wa Kakamega ambaye baada ya kuvutika na madhumuni ya kitabu hiki akawa tayari kukifasiri kwa lunga ya Kiswahili kutoka lugha ya Kiingereza. Na pamoja na hayo alijitolea kutoa msaada wa fedha kwa kupigisha chapa tafsiri hii. Pia namshukuru Sheikh Muhammad Munawwar, Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Ahmadiyya nchini Tanzania, kwa kutalii na kusahihisha tafsiri hii. Natumai wasomaji watasadiki kwamba kitabu kama hiki kinafaa sana. Baada ya kukisoma mnatakiwa kutafuta dini safi yenye mafundisho yaliyo bora kabisa na kuifuata. Nitawaomba wasomaji wa kitabu hiki wajipatie vitabu kuhusu dini ya Kiislam na kuvisoma kwa makini. Nina hakika, Mungu akipenda, wataona mwangaza.

Na mwishowe, ninamwomba Mwenyezi Mungu awaongoze ndugu Wakrito watoke katika janga la Kikristo na kushika dini ya haki ya pekee - Dini Tukufu ya Kiislam. Amin.

Sheikh Mohammad Ishaque Soofi, (B.A.)  
Amir na Mbashiri Mkuu,  
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya,  
Nairobi, Kenya.

Ahmadiyya Mosque,  
Fort Hall Road,  
Nairobi,  
Desemba, 1966.

## **MAELEZO YA KAFARA**

Wakristo wadai kwamba Mwenyezi Mungu ana mwana, aliye mwanawe wa pekee. Huyu mwana wa Mungu alijipa utu tumboni mwa Maria. Maria na mumewe Joseph seremala wakajulishwa hayo na Malaika na baada ya muda mwana wa Mungu akazaliwa sawa na mtoto wakibinadamu. Akalelewa kama mtoto wa wakibinadamu na alipokua akafanya miujiza. Mwana huyo ndiye Yesu aliyezaliwa katika Wayahudi ambao walimtesa na mwishowe wakamuua kwa kumtundika msalabani. Hivyo ndivyo mwana wa Mungu aliyejipa utu alivyokufa na akashukia jahanamu alikokaa siku tatu. Kisha akafufuka toka wafu na sasa yuko mbinguni akikaa kuumeni kwa Mungu.

Yesu ingawa hakuwa na kosa lolote, hata hivyo alivumilia mateso kwa ajili ya wanadamu ili kwa mateso yake awe kafara kwa dhambi za wanadamu. Kwahiyo, yule anayemkubali hawezi kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zake kwa maana Yesu amejitwika dhambi zote za watu. Wana wa Adamu wote ni wenye dhambi, ndivyo wasemavyo Wakristo. Adamu na Hawa walifukuzwa toka bustanini kwa ajili ya dhambi yao ambayo imerithiwa na wazao wao wote wanaozaliwa. Kwa sababu hii, Wakristo wanasema, ndiyo maana mwana wa Mungu hakuingia tumboni mwa Maria kwa njia ya mbegu ya mwanadamu, bali Maria alitunga mimba bila kuguswa na mwanamume yeyote wasije wakarithi dhambi ya Adamu kama wazao wake wengineo.

## **HAJA YA KAFARA**

Baada ya kueleza asili na maana ya kafara kama wasemavyo Wakristo, sasa nitaeleza haja yake kwa mradi wa fikara za Kikristo. Wakristo wadai kwamba mwanadamu ni mwenye dhambi na mwisho wa dhambi ni adhabu ya moto. Mwenyezi Mungu ni mwenye huruma

Mungu ni mwenye huruma na huruma yake yataraji kwamba mwanadamu aepushwe kutokana na adhabu hii. Lakini pia Mwenyezi Mungu ni mwenye haki na haki yake Mungu inataka itolewe adhabu. Je, ingaliwezekana huruma na haki kutumika pamoja? Mwana wa Mungu aliyekuwa hana kosa lolote akatoa jawabu la tatizo hili. Alitoa jawabu kwa kujitolea kuadhibiwa mahala pa mwanadamu na Mwenyezi Mungu akaridhia sadaka hiyo na kujitolea huko. Hivyo haki na huruma ya Mungu vikafanya kazi pamoja. Adhabu juu ya madhambi ya watu ikatolewa na watu pia wakawa huru! Adhabu ya dhambi za wanadamu ilikuwa nzito, lakini Yesu akajitwika. Kwahiyo kuteswa kwa mwana wa Mungu kwalinganishwa sawa na uzito wa adhabu ya jumla ambayo wangepewa wanadamu wote.

### **KANUSHO LA IMANI HII**

Hapa nataka kukanusha imani hii ya Wakristo. Kwanza nitatoa ushahidi wa akili na wa busara kuvunja itikadi hii.

Hoja ya kwanza ni ule ukweli wa kukosa kuthibitika katika vitendo. Hii itakuwa wazi zaidi ukifikiria mifano hii miwili ifuatayo: Nabii Musa alikuwa mtu pekee na kwa vyovyote alionekana dhaifu na mnyonge, lakini, alisimama imara mbele ya Firauni, mfalme wa Misri mwenye nguvu na majeshi. Nabii Musa alimwambia Firauni, "Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Watume wana wa Israeli pamoja nami. Ikiwa utakataa, basi ujue kwamba utashindwa." Hivyo Musa mbele ya Firauni alidai ya kuwa ni Mtume wa Mungu na pia akatabiri maangamio ya Firauni. Bishara hii kubwa ilitimia sawasawa na ukweli kwamba Musa a.s. alikuwa Nabii wa Mungu ukathibitika kwa vitendo.

Nabii mtukufu Muhammad s.a.w. alidhihiri katika Bara Arab. Waarabu wa siku hizo walikuwa wajinga waliopotoka na washenzi. Sayyidna Muhammad s.a.w. akawaambia "Nifuateni; mafundisho ya Qur`an Tukufu yatawaleteeni utamaduni na ustarabu, maarifa na elimu, nanyi mtakuwa mshindao." Hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa. Hii

ilithibitisha ukweli wa unabii wake kwa vitendo.

Mifano hii miwili ni ya kidini, hata hivyo napenda kuongeza mifano mingine ya kidunia. Kila Serikali hutunga sheria zenye kutoa adhabu kwa hatia na pia zipo sheria zenye kutunukia tuzo kwa mwenye kutenda kazi njema. Daima twashuhudia sheria hizi zikitimizwa kwa vitendo. Hebu natuangualie miaka 1900 iliyopita tangu Yesu alipotundikwa msalabani na tuone kama itikadi hii ya kafara inaongoza kwenye matukio yoyote yanayothibitika kwa vitendo.

Inasemekana kwamba Adamu na Hawa ndiyo waanzilishi wa dhambi ya asili hapa ulimwenguni na kuwa haiwezi kuondolewa kwa watu isipokuwa wanajifanya wenye kustahili wokovu kwa kuzingatia imani ya kafara ya Yesu. Yafaa kwanza tuone ni adhabu gani waliyopewa akina Adamu na Hawa kwa dhambi yao waliyofanya kisha tuone kama wale waaminio kafara ya Yesu wamesamehewa. Kutoka katika Biblia ni dhahiri kuwa adhabu aliyopewa Adamu kwa dhambi yake ni: "Kwa jasho la uso wako utakula." (Mwanzo 3:19). Na bibi Hawa naye akaambiwa, "Kwa uchungu utazaa watoto." (Mwanzo 3:16).

Sasa nauliza, Je, yupo Mkristo yeyote awezaye kusema kwa uaminifu kwamba yeye binafsi yu huru kutokana na adhabu hiyo ya hao Adamu na Hawa? Nani anayesema ya kuwa kwa kuzingatia imani ya kafara ya Yesu sasa yeye riziki hupata bila kuitolea jasho? Kadhalika yupo bibi yeyote wa Kikristo awezaye kusema kwa dhiti kwamba kuamini kwake kuwa Yesu ni mkombozi wake kumemwondolea uchungu wa kuzaa na kwamba yeye sasa huzaa bila ya uchungu? Hakuna Mkristo atakayeitikia `ndiyo` kwa maswali hayo hapo juu. Hii yaonesha wazi kuwa hizi kazi zetu tufanyazo kila siku zinaharamisha imani ya ndugu Wakristo juu ya kafara ya Yesu. Iwapo ni kweli kwamba Yesu alikomboa dhambi naye alibeba dhambi za watu na kwazo akaadhibiwa na watu wanachohitaji ni kumwamini tu, kwa nini basi wale wanaoamini Ukristo wanaendelea kupata adhabu ambapo Yesu alikwisha fika na kuondoa taabu hiyo? Hii inanifanya nise ya kuwa kafara ya Yesu haina manufaa yoyote, bali ni kitu cha kudhania tu na daima twashuhudia kinyume chake.

Pindi mtu anaamini na kukubali ukombozi wa Yesu, bila shaka mtu

huyo ana dhambi fulani fulani alizofanya kabla ya hapo na pia pana dhambi zingine awezazo kufanya baadaye. Ikiwa imani katika kafara ya Yesu ni kuleta msamaha wa dhambi hizo hapo italazimu asiadhibiwe kwa dhambi zake za zamani. Lakini matokeo ambayo daima tunaona yapo kinyume na hayo. Hebu tuseme mtu huyu aliyebatizwa alikuwa na hatia ya uzinifu na akawa na viini vya ugonjwa m`baya mwilini mwake, lakini maradhi yenyewe yawe bado kudhihirika; kwa mujibu wa imani ya kafara ni lazima Yesu aichukuwe adhabu ya dhambi hiyo. Hivyo, viini vya maradhi ya uasherati kama tego na kaswende vitalazimu vihamie mwilini mwa Yesu amkinge kutokana na shambulio la viini hivyo vya maradhi na kuwa salama salimini. Lakini hivi sivyo ilivyo.

Ukweli ni kwamba imani ya Mkristo katika kafara ya Yesu haimkingi kutokana na shambulio la viini hivyo vya maradhi ya uasherati na matokeo ni haya tu kwamba Mkristo huyo huwa windo zuri la maradhi ya tego na kaswende. Hii inaonesha kwamba imani katika ukombozi wa Yesu haimwondolei mtu dhambi alizozitenda kabla ya kubatizwa. Na kwa zile dhambi atakazozitenda baada ya kubatizwa, tunaona kuwa Wakristo wanapotenda maovu huadhibiwa kwayo kama watu wengineo. I wapi faida ya kafara? Kafara isiyoondoa dhambi za kabla ya ubatizo na zile za hatimae ina wokovu gani kwa watu?

Upotovu wa imani hii hakuna haja kutazama kwa darubini bali upo peupe. Imani ya kafara ya Yesu imeshindwa kabisa kutakasa nyoyo za wanadamu. Kila mwaka nchi za Kikristo idadi kubwa za wakosefu wenye hatia zinazidi. Ikiwa itasemwa ati hao hawafuati sheria, nasi tutaauliza, je, hii kafara ya Yesu matumizi yake kitu gani? Hata kama isemwe kwamba mradi wa imani ya kafara ni kuondolea mbali uwezo wa kutenda dhambi, sisi tunasema hii si kweli. Tukiacha kando wale Wakristo wa kawaida, hata hivyo tutabaki na orodha ndefu ya hatia chafu za wakuu wa Kikristo.

Inasemekana kwamba haki ya Mwenyezi Mungu haiwezi kutimizwa ila kwa njia ya kafara. Lakini ukweli ni kwamba imani hii inabatilisha haki. Yesu hakuwa na kosa lolote na ni udhalimu hasa kumtwisha mtu asiye na kosa mzigo wa mwenye dhambi.



Inawezekana kusemwa ya kuwa Yesu alimiliki uhai wake na kwamba alijitoa kuwa kafara kwa hiyari yake mwenyewe. Hoja hii itakuwa haina nguvu mbele ya Biblia. Biblia inatuambia kuwa hakupenda Yesu kifo cha kutundikwa msalabani, bali alimwomba Mwenyezi Mungu ili amwepushe na kikombe hicho cha mauti. Imeandikwa: "Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akaomba, akisema, Baba yangu ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe" (Mathayo 26:39). Tena pana kilio cha uchungu alicholia bwana Yesu kwa sauti kubwa, "Eloi, Eloi, lamasabaktani? Yaani Mungu wangu, Mungu wangu, mbona unaniacha?" (Mathayo27:46).

Dua hizi zaonesha dhahiri kuwa Yesu hakutoa uhai wake kwa hiyari kama watu wengine wanavyosema. Hata kama tukikubali kuwa alijitoa kwa hiyari, twakuta swali jingine moja ambalo ni hili: Ikiwa Yesu alimiliki uhai wake, je, Mwenyezi Mungu si mmiliki wa matendo yake mwenyewe? Si yeye mmiliki wa hazina za neema na mibaraka? Ikiwa Yesu aliweza kutoa uhai wake bila malipo, je, Mwenyezi Mungu hawezi kutoa ukarimu wake bure? Kuadhibiwa kwa Yesu kwa sababu ati ya dhambi za watu ni kitendo kinachokwenda kinyume na kanuni yake Mwenyezi Mungu, mwenye Haki.

Imani ya kafara inamfanya Yesu kuwa yu mdhalimu pia. Dhambi za mwanadamu zinakuwa za namna mbili. Mtu asipofanya wajibu wake kwa Mwenyezi Mungu au mwanadamu mwenzie. Mtu asipofanya wajibu wake kwa Mwenyezi Mungu, imani ya kafara ya Yesu itamwepusha adhabu. Mwanadamu alimwasi Mwenyezi Mungu, Mwana wa Mungu alijitwika adhabu ya uwasi huo na mwanadamu akawa huru. Lakini hebu natuangualie upande wa pili ambapo mwanadamu anamkosea mwenzake. Tuseme pana mtu aitwaye John ambaye ni mumini wa Yesu. Yesu anajitwisha dhambi zote za John pamoja na ile ya wizi wa saa. Henry ambaye ndiye mwenye saa anabaki akilia bila kupata saa yake. Je, sasa hamuoni kwamba upande wa Henry, Yesu amekuwa yu mdhalimu kwa kujitwika adhabu ya John? Hivyo kwa imani ya kafara, Yesu anapakazwa hatia ya udhalimu.

Inasemekana kwamba kama Mwenyezi Mungu angaliwasamehe watendao dhambi kwa huruma yake, bila ya kuwaadhibu kwa namna yoyote, basi wanalizama katika madhambi wakiamini kuwa Mungu atawasamehe tu. Lakini sisi tunaona ni itikadi hii ya kafara ya Yesu ndiyo imfanyayo mtu kuzidi kudidimia katika dhambi na uwasi. Njia ya kwanza inamweka mwanadamu katika hali ya wasiwasi kama Mungu atamsamehe au la, Katika hali hii mwanadamu ataogopa kumwasi Muumba wake. Lakini kwa mujibu wa njia ya pili, kafara ya Yesu, inamfanya kuwa na hakika kwamba yuko huru kutenda dhambi; maana Yesu keshachukuwa kila kitu, bali kitu kitakiwacho kwake ni kuamini. Kafara inampa mwanadamu nafasi ya kumwasi Mwenyezi Mungu. Ndiyo sababu watu wa Ulaya na Amerika wamezidi maasi na kuzama katika anasa za kidunia.

Mtu anapoadhibiwa kwa ajili ya dhambi zake kusudi la adabu hiyo huwa kumwongoa huyo mwenye dhambi. Lakini kusudi hili haliwezi kutimizwa iwapo mtu asiye na kosa lolote ataadhibiwa mahali pa yule mwenye makosa. Tufanyapo wema hutumfadhili Mwenyezi Mungu chochote. Na tufanyapo uwovu haimfikii dhiki yoyote. Ni sisi wenyewe tunaofaidi wema wetu au kupata hasara kwa sababu ya uwovu wetu. Laiti kama kutenda dhambi kwa wanadamu ni kumdhuru Mwenyezi Mungu, hapo tungelazimika kumridhisha kwa kumlipa na inatoshia hata mtu mwingine ajitolee kulipa badala yake. Lakini hivi sivyo ilivyo.

Imani ya ndugu Wakristo juu ya kafara inatukumbusha hadithi moja ya Mfalme Chaupat. Siku moja mhalifu aliletwa kwa mfalme Chaupat ili ahukumiwe. Mfalme aliamuru mhalifu huyo anyongwe. Mfalme alipojulishwa ya kuwa upana wa kitanzi cha kamba ya kunyongea ulizidi shingo ya mhalifu, mfalme akasema, "basi mtu mnene anyongwe badala yake". Kwa ufupi upotovu wa itikadi ya kafara ya Yesu unakuwa wazi kwa vile kunamfanya Mwenyezi Mungu aonekane mwenye kiu sana ya kuadhibu watu hata kama hawana kosa.

Wakristo wanasema mshahara wa dhambi ni mauti. Husema hivyo wakifuatia mamlaka ya vitabu vyao. Kwa mujibu huu ingefaa basi watu wote ambao mishahara ya dhambi zao imelipwa na mtu mwingine, wao wasife katu. Maana inajulikana kwamba kifo cha Yesu kilifidia

dhambi za wale wanaomwamini, hivyo wafuasi wake hawangekufa kwamwe. Lakini mambo yamekuwa kinyume. Sisi tunawaona Wakristo wakikabiliwa na mauti kama watu wengine wasiokubali kafara ya Yesu. Hii inaonesha kwamba kafara ya Yesu haikuwafaa chochote Wakristo hao.

Kusema kweli Wakristo hawakuelewa sifa hizi mbili: Haki na huruma. Wamechukuwa huruma kuwa kinyume cha haki, ambapo kinyume cha haki si huruma bali ni dhuluma. Maana ya haki ni kwamba mtu atendewe uadilifu. Kwa kuwa imani ya Kikristo imejengwa juu ya wazo kwamba huruma ni kinyume cha haki, basi inakuwa wazi kuwa wao wamesimama juu ya msingi ulio mbovu sana na usiofaa hata chembe.

Inasememwa na Wakristo kuwa hapana njia nyingine yoyote ya kuleta msamaha wa dhambi ila kafara ya Yesu. Lakini tunaona Mwenyezi Mungu amejaalia uwezo wa kuondoa dhambi katika maumbile. Mtu alapo chakula kibaya huwa anavunja kawaida na bila shaka ataugua **maradhi**. Lakini akigeuka na kutumia dawa ifaayo, yumkini atapata ahuweni na maumivu yote yataondoka. Hii ni njia ya ya kimaumbile kundoa maradhi yatokanayo na kuhalifu sheria na kanuni za maumbile. Lakini je, ni nani aliyemwona daktari amejiua mwenyewe kwa sababu ya kuponyesha wagonjwa wake? Bila shaka daktari hodari hutafuta dawa na kuanza kuwatibu wagonjwa wake. Ni daktari mzembe sana anayejitumbua kisu ili wagonjwa wake wapate afya.

Kafara ya bwana Yesu kwa kuokoa watu, tunaona inakwenda kinyume na kanuni zote za Mwenyezi Mungu. Hapa duniani daima tunaona, kwa mfano, vita. Vita askari wa kawaida hapigana safu ya mbele kabisa, nao maofisa huwa nyuma ya hao hali amiri jeshi huchukua mahali pa usalama zaidi,,ambapo mfalme huwa yupo salama salimini ngomeni mwake. Askari hutoa maisha yao kwa ajili ya kapteni, naye kapteni kwa ajili ya Kanali na huyu naye kwa ajili ya Jemedari na Jemedari kwa ajili ya Amiri jeshi. Amiri jeshi au mfalme hawezi kutolewa kafara ili kuokoa maisha ya askari. Ni fundisho la ajabu tu la hawa Wakristo kutuambia Yesu ambaye wanamwamini kuwa mwana wa Mungu alikufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu wasiyo na thamani

yoyote wakilinganishwa na Mwana wa Mungu.

Wanyama kama vile ng'ombe na mbuzi huchinjwa kwa ajili ya manufaa ya mwanadamu. Mapanya waenezao tauni huuawa ili maisha ya mwanadamu yasiwe katika hatari. Hatujaona mwanadamu anakufa ili kuhifadhi maisha ya wadudu. Basi mwana wa Mwenyezi Mungu awezaje kujifanya kafara kwa ajili ya wanadamu? Ndipo tunaposema imani ya kafara ya Yesu ni kinyume na akili, kinyume na uchunguzi na kinyume na kanuni za maumbile.

Ni uwongo kusema ya kuwa wanadamu wote huzaliwa wakiwa na dhambi. Ulimwengu mzima hufikiria watoto hususan wachanga kuwa ni malaika, yaani hawana dhambi yoyote. Yesu pia aliwaita watoto waende kwake. Akasema, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa kuwa watu kama hao ufalme wa Mungu ni wao" (Luka 18:16). Kwa nini hakusema ufalme wa mbinguni ni wa yule anayeamini kafara yake?

## **DHAMBIBI ZAONDOLEWA NAMNA GANI?**

Kabla ya Yesu kufika njia ya kusamehewa madhambi ilikuwa maombi na kutorejea tena katika matendo mabaya. Katika wakati wa Musa a.s. tunasimuliwa na Biblia kwamba wana wa Israeli walipoona Musa a.s. anakawia kutoka huko mlimani, basi wakajitengenezea ndama wa dhahabu wakamuabudu. Mwenyezi Mungu akawakasirikia wana wa Israeli. Nabii Musa a.s. akasikitishwa sana na jambo hilo. Upande mmoja akaamuru watu wake kuuwa kwa mikono yao watu wale walioleta kufuru na upande mwingine akapenda yeye mwenyewe awe kafara kwa ajili ya wafuasi wake, yaani auawe. Lakini Mwenyezi Mungu akamjibu akasema, "Mtu yeyote aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta katika kitabu changu" (Kutoka 22:33).

Hii inatujulisha mpango wa Wakristo juu ya kafara ni jambo ambalo wao wenyewe wamelipanga wala halipo katika kanuni ya Mwenyezi Mungu. Mungu hawaadhibu wasio na makosa mahali pa wale wenye

dhambi. Ingawa Musa a.s. aliridhia kujitoa kafara kwa ajili ya watu wake, lakini Mwenyezi Mungu alikataa ombi hilo. Kama kafara ya mtu ndiyo inayotakiwa baada ya watu kutenda dhambi, basi Mwenyezi Mungu hangeona ombi la Musa a.s. kuwa halina maana. Bali Mungu angeweza kumwambia Musa a.s. kwamba kazi hiyo amejitwika Yesu. Mwenyezi Mungu hakupata kumwambia Musa a.s. au nabii yeyote kwamba mwanawe ataadhibiwa kwa sababu ya dhambi za watu. Ni ajabu tu leo tunaambiwa na Wakristo ati Yesu ni kafara ya dhambi za watu!

Wakristo hawawezi kukana ya kuwa manabii wote wameokoka. Je, manabii hao waliokolewa na kafara ya Yesu iwapo walifika hata kabla ya Yesu mwenyewe? Hakuna dawa ya kusamehewa ila kuomba toba tu. Mwenyezi Mungu alimwambia nabii Suleiman hivi: "Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu watajinyenyekesha na kuomba na kunitafuta uso na kuziacha njia zao mbaya, basi nitasikia toka mbinguni na kuwasamehe dhambi zao." (2 Mambo ya Nyakati 7:14). Mwenyezi Mungu hakusema watu hawawezi kusamehewa dhambi zao ila kwa kafara ya Yesu. Kwa nini watu wabaki kunga`ang`ania imani hii? Kwa nini ndugu Wakristo hawawezi kufikiri kidogo na kuangalia mambo yalivyo?

Yesu mwenyewe anazumgumza juu ya wokovu, anasema, "Ingieni kwa kupita mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache" (Mathayo 7:13:14). Katika maneno haya Yesu anaonesha njia ya wokovu kuwa ni yenye taabu na yenye kuhitaji uvumilivu na kujinyima. Lakini tuonavyo njia ya kafara si ngumu wala si nyembamba. Kwa upande mwingine njia ya kafara ni mlango ulio mpana sana. Fanya upendavyo na imani ya kafara itakuondolea dhambi zako zote. Hushurutishwi kufuata sheria yoyote, bali kukiri kafara ya Yesu tu!

## DALILI ZA KAFARA ZINACHUNGUZA

Haitakuwa vibaya kutaja hapa vifungu vya maneno ya Agano la Kale na Jipya ambavyo Wakristo huvichukua kuwa vyenye kusaidia fundisho lao la imani ya kafara! Yesu alisema ya kuwa ni mchungaji mwema aliyeyatoa maisha yake kwa ajili ya kundi lake. Tena, inasemakana, alipokaribia kusulubiwa aliketi karibu karibu na hao thenashara ambao alikula nao na akachukua mkate akaubariki. Akawapa wanafunzi naye akasema, watwae wale na ya kwamba huo ndio mwili wake Yesu. Kadhalika inasemwa Yesu alitwaa kikombe na kuwaambia wanafunzi wake wanywe, kwa maana hiyo ndiyo damu yake ya Agano Jipya imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa kuondoa dhambi zao!

Hii ndiyo misemo ya pekee ambayo Wakristo huchukua kusaidia imani yao ya kafara. Hata kama misemo hiyo imeaminiwa ya kuwa ni ya asili katika Biblia, haihakikishi kuwa Yesu aliadhibiwa kwa ajili ya wanadamu wote. Bali meneno hayo ni ya kawaida kwa kiongozi yeyote wa kiroho. Kila nabii na kila mtume huumizwa kwa ajili ya watu wake. Si hayo tu, bali huvumilia kuumizwa hata na watu wake pia. Lakini kwa nguvu za Sala na maombi, mizigo ya dhambi ya watu huondolewa. Kama watu hawangezama dhambini, Mwenyezi Mungu hangeleta mwonyaji.

Ni kweli Yesu alivumilia maumivu kama walivyovumilia manabii wengine. Na kwa juhudi ya sala na maombi watu wa nabii Isa a.s. (Yesu) walipata matunda mema kama vile sala na dua za Musa a.s. zilivyoondoa na kuwaokoa watu wake kutokana na maangamio.

Kadhalika iwapo Yesu alifika kuwaokoa watu wote wa ulimwengu kwa nini katumia kwa "ajili ya wengi" "Kwa ajili ya wengi" inaonesha Yesu alikuwa anaongea juu ya watu wa taifa lake pekee ambao kwa ajili yao Yesu alitumwa kuwaongoza na alipata taabu kuwaonesha njia ya kufika kwa Mwenyezi Mungu.

Imeoneshwa kuwa pana vifungu kadhaa katika Agano la Kale vyenye kupotoa imani hiyo ya kafara. Hata hivyo Wakristo hudhania kuwepo maneno fulani katika Agano la Kale yenye kusaidia imani yao.

Lakini ukweli ni kuwa maneno yenyewe hayo hayamhusu Yesu wala kafara yake. Kifungu kimoja kinachodhaniwa kuunga mkono imani yao ya kafara kinasema: "Angalia siku zinakuja, asema BWANA, nitakapofanya Agano jipya na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda. Si kwa mfano wa Agano lile nililofanya na baba zao ..... Baada ya siku zile, asema BWANA, nitatia sheria yangu katika sehemu zao za ndani na katika nyoyo zao nitaandika, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu ....Nitasamehe uwovu wao, wala dhambi yao sitaikumbuka tena" (Yewremia 31:31-34).

Wakristo huwekea umuhimu mkubwa juu ya aya ya mwisho katika kifungu hicho cha maneno wakidhanika kuwa ndiyo yenye kuhakikisha imani yao ya kafara. Lakini wanasahau kwamba katika Agano la Kale mmeandikwa ya kuwa kulikuwapo msamaha wa dhambi. Msamaha huo ulifika baada ya watu kutubu na kuombewa na nabii wao. Hakuna kitu kigeni katika aya hiyo kinachoweza kutufanya tufikirie kwamba pamedokezea au kugusia kafara ya Yesu. Kama ingesemwa kwamba hapo mwanzo Mwenyezi Mungu hakusamehe dhambi kabisa, yumkini pangekuwapo sababu ya kufikiria kule kutajwa kusiko kwa kawaida kwa njia ya kuleta msamaha wa dhambi. Lakini tunaona kuwa msamaha wa dhambi ulikuwapo miogoni mwa Israeli kabla na baada ya aya hiyo. Basi kwa nini tufikirie kuwa mujibu wa msamaha wa dhambi uliotajwa katika aya hiyo ni kafara ya Yesu?

Ingawa ni hivyo, yapo maneno yenye kuashiria tukio la baadaye .Moja ya aya hizo yasema: "Nitafanya Agano jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda. Si kwa mfano wa Agano lile nililofanya na baba zao." Akieleza juu ya aya hii Mwenyezi Mungu anasema, "Nitatia sheria yangu katika sehemu zao za ndani." Kwa mujibu wa imani ya Kikristo ni dhahiri Yesu hakuleta sheria yoyote, lakini hakika ni kuwa aya hizo zatabiri kuletwa kwa sheria mpya. Sheria hiyo moja ni Qur`an Tukufu aliyofunuliwa Nabii Muahmmad s.a.w. ambayo inawakumbusha wana wa Israeli bishara ambayo hivi punde tu imesomwa hapo juu. Qur`an Tukufu inasema: "Enyi wana wa Israeli, ikumbukeni neema yangu niliyowanemesheni nayo na itekelezeni ahadi yangu nitatekeleza ahadi yenu na niogopeni mimi tu" (Qur`an Tukufu 2:41). Aya hii ina mradi kwamba wana wa Israeli waikubali sheria

hiyo mpya waliyoahidiwa na Mwenyezi Mungu atawatekelezea ahadi zake zote alizofanya katika Agano la Kale.

Wale waliokubali wito huu si kwamba walipewa neema za mbinguni tu, bali hapa duniani pia walipewa heshima na wakawa watawala na wafalme wenye nguvu. Waafghani na ndugu zao. Wakashimiri siku hizi waaminiwa kuwa wazao wa Israeli ambao ni jumla ya yale makabila kumi na mawili yaliyopotea. Hivyo kati ya hao wana wa Israeli waliopotea waliikubali sheria mpya (Qur`an Tukufu) na matokeao yake yakawa kwamba Mwenyezi Mungu hakuzikumbuka dhambi za baba zao. Lakini wale waliokana kupokea sheria hiyo mpya, mpaka sasa wako chini ya ghadhabu za Mwenyezi Mungu.

## **USHAHIDI WA TAREHE WAIPINGA KAFARA**

Nimekwisha kuonesha kwamba Biblia haina ushahidi wowote juu ya imani ya Wakristo ya Kafara ya Yesu. Sasa yafaa tuchungue ukweli wa itikadi hii katika msingi wa historia. Wokovu wa ulimwengu mzima yasemekana wategemea juu ya imani kuwa Yesu alikufa msalabani na baada ya hapo kutoka kwake katika wafu na kupaa ni matukio ya shani katika historia ya ulimwengu ya kuwa wokovu wa watu unategemea matukio hayo makuu. Lakini sisi twasema kuwa ikiwa kifo cha Yesu msalabani kilikusudiwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwakomboa watu wote wa ulimwengu, basi kifo hicho ingefaa Mwenyezi Mungu akifanye wazi machoni pa walimwengu. Maandiko ya historia yangepaswa kutoa ushahidi juu ya ukweli kwamba Mwana wa Mungu alizuru ulimwengu huu karne fulani na ya kuwa alikufa msalabani kwa ajili ya wenye dhambi. Lakini sasa ushahidi tulio nao ni ule wa Injili tu ambao humo pia jambo hili halimo katika sura ya ukweli wala hautaji kafara ya Yesu. Kadhalika hauwei kupinga hoja kuwa maneno haya "Alitoka kwa wafu" yanaweza kuwa na maana kwamba alipata fahamu baada ya kuzimia.



Injili kama usome kwa makini wazi itakuonesha dalili nyingi kuwa Yesu aliepuka kifo cha laana cha msalaba. Linge kuwa jambo refu sana kutoa hapa ushahidi wote wa Injili unaothibitisha kuwa Yesu hakufa msalabani. Swali lifuatalo linatosha kuonesha upuuzi wa dhana ya Wakristo kuwa Yesu alifufuka toka wafu na akaruka kwenda mbinguni. Ikiwa ni hivyo kwa nini Yesu alipofufuka toka wafu alijifichaficha akachelea asije akakamatwa? Kwa nini alificha lile tendo lake la mwisho, lile la kupaa mbinguni lisifanyike mbele na machoni pa Mayahudi? Ingawa nyota haina uhusiano wowote na ukombozi wa wanadamu, lakini iangukapo hushuhudiwa na watu wengi hata kama hawakuwa wenye kungojea. Bali jambo la ajabu ni ukweli kwamba hapana hata mtu mmoja katika wasiomwamini Yesu aliyeshuhudia kupaa kwa yule aliyefufuka toka wafu. Hapana mtu mmoja anayedai kwamba aliona mwanadamu akivurumika kuelekea mbinguni, iwe pekee au kusindikizwa na kundi la malaika. Hata maroketi yanaporushwa angani watu hupashwa habari mapema nao wanayaona. Mbona Yesu hakutangaza?

Ukweli ni huu tu ya kuwa Yesu hakusafiri kwenda mbinguni. Kama hadithi hii ya kusema Yesu amepaa mbinguni ni kweli, basi mradi wake ni huu kwamba baada ya kuwaaga wanafunzi wake chini ya mlima, Yesu alipanda mlima huo akinuia kufanya safari ndefu. Kule juu milimani mawingu yalitanda, yakielekea mbinguni. Hapo wenye kukisia wakasema Yesu amepaa mbinguni! Kwa wanafunzi wa Yesu kusema hivyo ilikuwa sawasawa maana walikuwa na nia ya kuwazuia Mayahudi wasimfuate Yesu wakamshika tena mara ya pili.

Wakristo wa madhehebu mengine wanaamini kuwa Yesu aliishi duniani miaka 11 baada ya kusulubiwa. Wengine wanasema la, bali aliishi miezi kadhaa. Waliobaki wananena, sivyoyaliishi siku 40 tu. Swali ni hili: Yesu alikuwa na haja gani kujifichaficha baada ya kusulubiwa? Alikuwa ameshasulubiwa tayari, alikwisha onja kifo kile alichofikia, akaingia Jahanamu na kazi ya ukombozi ikakamilika; kwa nini tena aliendelea kuwa na udhaifu wa kibinadamu? Kwa nini hakuwaendea Mayahudi na kuwaonesha makarama yake na uwezo alikuwa nao wa Kiungu ili nao wakamwamini?

Ili kukanusha imani potevu ya Kikristo, Qur`an Tukufu inashambulia kiini hasa cha dini hiyo. Imethibitika bila taabu kuwa Yesu hakufa kifo cha laana cha msalabani na ya kuwa hakuwa mwana wa Mungu. Na hii inatosha kuvunjilia mbali imani ya Kikristo juu ya ukombozi wa kafara ya Yesu. Isitoshe, Qur`an Tukufu inakanusha imani ya aina hii na kusema, "WALA NAFSI YOYOTE HAICHUMI (UBAYA) ILA NI JUU YAKE, WALA M`BEBAJI HATABEBA MZIGO WA MWINGINE.'" (6:165)

Haikuwa lazima hapa kutaja imani ya kafara ya Kikristo, kwani ikithibitishwa kwamba Yesu alikuwa mwanadamu na kuwa hakufa kifo cha laana kile cha msalabani, bali alikufa kifo cha kawaida; yale mawazo yote ya kipumbavu hususan ya kafara yake, hayo yatafutika kabisa katika akili za watu.

## **KWA NINI TWAKATAA**

Kama kuna manufaa yoyote katika itikadi ya kafara, bila shaka tungalikubali. Lakini mbali na kutunufaisha imani hii, tunatokomezwa kwenye matokeo maovu mno. Hapa upo mfano wa uwovu huo. KWANZA: Imani ya kafara ni kinyume na akili zetu. Akili ya mwanadamu inakataa wazo hili kwamba John ajipasuwe tumbo lake ili amponyeshe Henry maradhi ya kichwa.

PILI: Kukubali imani ya kafara ya Yesu ni sawa na kukataa Agano la Kale, kwani inaonesha njia nyingine ya kuleta msamaha wa dhambi. TATU: Ikiwa tutakubali kafara ya Yesu, basi ni lazima tukubali kuwa Yesu alilaaniwa, hali laana inamsukuma yule aliyelaaniwa mbali na Mwenyezi Mungu na kumsogeza karibu na shetani. Laana ni jina tu lisilo na mujibu wake. Waila laonesha hali ya roho na ambayo ni dhambi kubwa kuitaja kwa vyovyote kuwa nayo Nabii wa Mungu. Wakristo wanaposema kuwa Yesu alilaaniwa, wao hawatishwi na maana ya laana.

NNE: Itikadi ya kafara inamfanya Mwenyezi Mungu kutokuwa mwenye Haki, anaweza kumwadhibu mtu ambaye hakufanya kosa lolote.

TANO: Kukubali imani ya kafara ni kukataa kuwa Mwenyezi Mungu ni mwenye huruma, kwani hakutosheka na kutubu kwa watu wake, bali aliona bora kumtoa Yesu aje amwadhibu kwa ajili ya dhambi za wanadamu.

SITA: Ikiwa kafara ni njia ya kweli, basi Manabii wote waliopita kabla ya Yesu wote watakuwa hawana ukweli, maana wao walifundisha njia nyingine ya kupata wokovu.

SABA: Ikiwa kafara ni kweli, basi watakatifu walioleta dini zote hapo mwanzo watakuwa na makosa sababu hakuna hata mmoja wao aliyefundisha itikadi hii.

NANE: Ikiwa Kafara ni kweli, baraza zote za sheria katika nchi za Kikristo zina hatia ya dhambi ya uwovu mkubwa, kwani hazitofautishi Wakristo na wasiyo Wakristo. Haifai kuwadhibu wote sawa bila kujali kwamba dhambi za wale Wakristo zilifidiwa na kifo cha Yesu na kwazo akaadhibiwa.

TISA: Kafara imewafanya Wakristo wa hali zote kuwa sawa. Kwa mfano mmoja akiwa na 99 kwa mia ya matendo yake maovu, na mwingine 50 kwa mia na mwingine moja tu kwa mia; lakini Kafara inaondoa dhambi zao zote na wote wanawekwa katika daraja moja ya usafi. Hivyo wale waliofanya wema zaidi wanakuwa sawa na wale ambao hawakufanya wema wowote. Hii si haki abadan. Mtu awezaje kuamini itikadi yenye udhalimu kama huu?

KUMI: Ikiwa Kafara yatosha, basi hapana haja ya kusali, maana wokovu unapatikana tele kwa kuamini kafara tu. Yote tunayohitaji kufanya ni kuamni ukombozi, na sala haina lazima. Hili ni ovu kuu linalotufanya tuikatae imani ya kafara. Kwani Sala ndiyo uhai wa waaminio. Mcha Mungu anawezaje kuishi bila ya kusali? Yesu mwenyewe aliwafundisha wanafunzi wake kusali na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa manabii wote wa Mwenyezi Mungu.

KUMI NA MOJA: Itikadi ya Kafara inamfanya mtu kuamini kuwa hata Mungu alikufa. Wakristo wanamwamini Yesu kuwa Mungu.

**KUMI NA MBILI:** Imani ya Kafara ina maana kwamba Mwenyezi Mungu ni mwenye kiu ya damu na hatosheki na chochote ila damu ya mwanadamu. Mungu ni lazima apate damu wala si kingine, haidhuru damu hiyo iwe ni ya mwenye dhambi au asiye na dhambi.

**KUMI NA TATU:** Imani hii haina ushahidi wa historia.

## **CHIMBUKO LA KAFARA**

Itikadi ya Kikristo ya kafara inapingana na fikira za kawaida na wala haisaidiwi na Injili au kauli yoyote ya Yesu. Daima watu wanauliza chanzo cha imani hii ni nini? Ukweli ni kwamba Yesu na wanafunzi wake wote ni wageni katika imani hii iliyovumbuliwa na Paulo. Ilikuwa ni mwisho wa karne ya jana ambapo Injili mpya ilienezwa huko Amerika. Injili hiyo inajulikana kwa jina la **THE STORY OF CURCIFIXION BY AN EYE WITNESS**, yaani, maelezo ya kusulubiwa na shahidi aliyeona kwa macho. Mwandishi wa Kitabu hicho amesema wazi kuwa Yesu hakufa msalabani na kwamba alihamia nchi nyingine baada ya kusulubiwa kwake.

Shabaha ya Mayahudi, kama nilivyosema hapo mbele, ilikuwa kwamba wamsulubu Yesu ili aonekane kuwa mtu aliyelaaniwa kama ilivyoandikwa katika Biblia, "Kwani aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu." (Kumbukumbu la Torati 21:23). Hivyo wanafunzi wa Yesu walitatizwa. Kukubali kuwa Yesu alikufa msalabani wanaona atafanywa amelaaniwa. Kusema kuwa Yesu aliponyoka na yupo safarini kuelekea nchi nyingine ya mbali, hilo lilikuwa jambo la hatari kubwa, maana serikali ingeweza kumshika tena Yesu na kumtia msalabani na kumwua. Kwa ujanja Paulo akawabunia hila nao hawakukataa kwa sababu waliliona hilo ni njia ya pekee ya kuondoa tatizo lao gumu sana. Katika maarifa yake, Paulo alikisia kuwa ni kweli Yesu alikufa msalabani na kulaaniwa. Lakini hakuwa na kosa bali alijitwika laana hiyo kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Hivyo kifo cha msalaba hakikuwa cha fedheha, bali ni jambo lenye sifa njema na

fadhila! Hapo basi ndipo ndugu Wakristo wakawa na kitu cha kujisifia wakapata jibu la kuwaeleza Mayahudi.

Uvumbuzi huu wa Paulo ingawa u hivyo, kwa kweli hapo mwanzo ulikuwa kama ngao ya Wakristo ya kuingia matusi ya Mayahudi, lakini pole pole iligeuka kinga hiyo kuwa imani ya ukombozi ambayo hivi leo inahubiriwa kote ulimwenguni. Kwa ufupi, Yesu haikuwa afundishe imani ya kafara hii inayosemwa juu yake wala hao wanafunzi wake pia hawakueleza habari hizi. Bali mwalimu wa imani hii alikuwa Paulo hata imekuwa kwamba Wakristo wenye kufikiri hujiuliza je, Ukristo huu wa leo ni wa Yesu au ni wa Paulo?

Siku chache zilizopita mtaalamu mmoja wa Kijerumani aitwaye Dr. Arnold Meyer aliandika kitabu juu ya Ukristo na imani zao kadha zilizotiwa humo. Kitabu hicho kimefasiriwa kwa Kiingereza na kinaitwa "Jesus or Paul?" Yaani, Yesu au Paulo? Ndani ya kitabu hicho, mtaalamu huyo wa Kijerumani amethibitisha kwamba "uungu wa Yesu na Kafara yake ni imani ambayo mwanzo wake ulitokana na ujanja wa Paulo na ambayo Yesu na wanafunzi wake hawakujua aslan."

Mayahudi kwa sababu ya uwadui wao na chuki walimchukulia Yesu kuwa mtu aliyelaaniwa ambaye mwisho wake ungekuwa moto mkali wa Jahanamu. Wakristo nao wakisukumwa na tamaa yao ya kupata wokovu kwa urahisi wanakubali kuwa Yesu alilaaniwa na akaingia Jahanamu. Hivyo maadui na marafiki wa Yesu wote wanaungana pamoja na kumtumbukiza motoni. Mwenyezi Mungu ampe Muhammad, Mtume Mtukufu wa Islam neema na baraka zake nyingi, ambaye ndiye aliyemwokoza Yesu katika shimo la moto na kuthibitisha Yesu hakuwa mtu aliyelaaniwa, bali ni nabii wa Mwenyezi Mungu. Nabii Muhammad s.a.w. si kwamba alimwokoza Yesu tu, lakini hata Bi Mariamu pia alimwondolea mashitaka maovu aliyowekewa na Mayahudi hata imekuwa siku hizi Wakristo wanaposhindwa kupata thibitsho la usafi wa tabia ya Yesu hukimbilia Qur`an Tukufu ambayo ina ushahidi murua. Qur`an Tukufu ndiyo iliyomfanya Yesu awe mtakatifu na mtawa pamoja na mama yake. Kwa ufupi, Paulo ndiye aliyepanda Ukristo huu wa leo kwani ndiye aliyejua kusoma na kuadika. Ama wanafunzi wengine wa Yesu hawakuelewa chochote.

Akiongea juu ya ukombozi, mwanachuoni mmoja Mkristo aliyeandika kitabu cha "History of the Christian Religion and the Church" akiri kwamba "itikadi ya kafara halikuwa jambo lililokuwa na umbo dhahiri mpaka kwenye karne ya kumi na mbili. Karne hiyo ni muhimu mno katika historia ya kuvumbuliwa kwa imani hii." (Jalada la 1 B, ukurasa 497 mtungaji Bwana Meander).

Hapa pana swali la kawaida je, kuna dawa gani kwa dhambi? Kwani maisha maovu ni heri mauti. Ni bahati njema kwa mwanadamu, maana tatizo hili lilikwisha kufumbuliwa zamani na mwanzilishaji wa Islam, Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. kwa njia yenye kukubalika. Kufuatia kanuni za maumbile nasi tumekwisha kushuhudia kurekebisha kwa njia hii katika hali yake ya usafi na Seyyidna Ahmad wa Qadian aliye mfuasi mwaminifu wa Mtume Muhammad s.a.w. si katika madai yake yenye kukubalika tu, bali kwa ukweli uliohakiki juu yake na ishara zake zenye nguvu.

Hadhrat Ahmad a.s. amesema "Tangu kuumbwa ulimwengu pamekuwapo na kinga moja tu kwa dhambi. Mwanadamu alipotafakari juu ya hoja zinazokubalika na ishara zilizo wazi na kupata hakika ya kuwapo kwa Mwenyezi Mungu na kuthibitisha kwa yakini kuwa ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ni moto uunguzao, hapo ndipo unapopata mwangaza wa utukufu toka mbinguni unaomfunulia kwamba Mwenyezi Mungu ndiye hasa asili ya raha na malipo mema. Au kwa vingine, Mwenyezi Mungu hujidhihirisha kwenye moyo wa mwanadamu. Hivyo, awezaye kuepuka dhambi ni yule tu aliye na yakini juu ya kuwapo kwa Mwenyezi Mungu na ambaye daima huzingatia kwa mapenzi na kumwogopa Yeye pekee.

"Uovu na elimu ya yakini haviwezi kukaa ndani ya moyo mmoja. Elimu ya yakini ndiyo ponyo la pekee kwa maradhi yako ya dhambi. Kusulubiwa kwa yeyote hakuwezi kukuondolea mzigo wako wa dhambi. Damu ya yeyote haiwezi kukuzuia usitawaliwe na tamaa mbaya za kimwili. Vitu kama hivi havina uhusiano wowote na wokovu wa kweli. Omba, jaribu kuelewa hakika na jifunze kutafakari juu ya ukweli. Yajaribu haya kama vile unavyojaribu mambo mengine ya kidunia na kisha utakuja fahamu kwamba elimu ya yakini ndiyo

mwangaza wa pekee unaoweza kupenya ndani ya moyo wenye giza. Elimu ya yakini ndiyo dawa yenye nguvu za kusafisha maumivu na maradhi ya kutojua." (Review of Religions 1902).

Mwanadamu anapojitahidi katika imani yake na kutenda matendo mema na anakuwa tayari kumtii Mwenyezi Mungu na mitume wake, basi rehema za Mwenyezi Mungu huwa pamoja naye na kumwongoza katika njia iliyo sawasawa. Katika kitabu kitukufu cha Qur`an Mungu anasema, "Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na mtume, basi hao ni miongoni mwa wale aliyowaneemesha Mwenyezi Mungu - Manabii, Masadiqi, Mashahidi na Masalih na hao ndiyo marafiki wema" (Sura 4:70). Tena baada ya kufanya kosa kwa sababu ya udhaifu wa kibinadamu mtu anapasa ajiepushe na dhambi zile kubwa, sehemu zile ndogo zilandamanazo na dhambi hizo zinasamehewa. Kama mfano, mtu amtazame mwanamke kwa kumtamani, halafu akurubie, kishapo anuie kumjua. Katika hali hizi zote mtu huyo anahesabiwa kama atenda dhambi. Lakini iwapo baada ya kupitia katika hali hizo zote za mwanzoni akatubu na kuacha kuendelea mpaka kileleni, bali akafuata msamaha wa Mwenyezi Mungu; sehemu hizo zote za mwanzoni husamehewa. Huu ndiyo mlingano ulio sawa kati ya haki na maumbile ya mwanadamu. Hayo yameelezwa katika sura 4:32,. Qur`n Tukufu pia inasema "hakika mema huyaondoa mabaya" (11:115). Ndiyo kusema usafi huondolea mbali uchafu.

Dunia hii yetu ni mfano wa ulimwengu wa kiroho na inavyo vielelezo vingi vyenye kutuongoza kwenye dunia ya Kiakhera. Hivyo kutokuwa na dhambi pekee hakumfanyi mtu kuwa mkombozi wa wanadamu. Kuna sifa nyingine nyingi zinazohitajika katika cheo hicho. Nabii wetu Mtukufu Muhammad s.a.w. si kwamba hakuwa na dhambi tu, bali zaidi ya hivyo yeye alikuwa na sifa zote za lazima kuwa mwokozi. Qur`an Tukufu inamtangaza Mtume s.a.w. kuwa ni mtu asiye na dhambi, hali nabii Isa a.s. (Yesu) haikuwa hivyo. Ingawa manabii wote wa Mwenyezi Mungu wana usawa katika hali ya kutakaswa na madhambi.

Kule kuwapo kwa mtu mmoja tu mtakatifu miongoni mwa watu, huwa ni sababu ya uombezi kwa wanadamu. Kwani Mwenyezi Mungu huzuia adhabu yake mpaka mtakatifu huyo atoweke miongoni mwa watu hao. Agano la Kale linalo mfano katika jambo hili. Nabii Muhammad s.a.w. alikuwa mwanadamu mtiifu na mtimilifu. Kulikuwa na mwungano mkubwa kati yake na Mwenyezi Mungu. Mtume Muhammad s.a.w. alizama katika mapenzi ya Mungu hivi kwamba matendo yake yote, hata kifo chake kilikuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Nafsini mwake Mtume Muhammad s.a.w. hamkuwa na viungo vya kidunia na roho yake ilianguka mbele ya Mwenyezi Mungu kwa mapenzi kamili yaliyojaa moyoni. Kwa njia hii Mtume Muhammad s.a.w. ametekeleza sharti moja iliyo ya lazima kwa mwombezi. Sharti lile ya pili pia Mtume Mtukufu amelitimiza kama inavyothibitishwa na Qur`an kwa kusema, "kisha akakaribia na akateremka na ndipo akawa umbali wa pinde mbili au karibu zaidi" (Sura 53:9-10). Ndiyo kusema nabii Muhammad s.a.w. katika hali ya kiroho alinyanyuka juu kwa ukaribu zaidi kama inavyowezekana akipitia kila daraja katika kumkurubia Mola wake hata akafikia upeo wa mwisho wa hali yake ya kibinadamu na ile sehemu yake timilifu ya mapenzi yake juu ya mwanadamu.

Kwa upande mmoja alikuwa na mapenzi ya upeo wa juu ya Mwenyezi Mungu na upande mwingine alikuwa na huruma ya upeo wa juu ya wanadamu. Hivyo Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alikaribia sana ule mpaka baina ya vipeo vya mwisho vya utakatifu na uwanadamu na akawa mfano wa nguzo baina ya matao mawili. Bila shaka Mtume Muhammad s.a.w. alikuwa kielezo halisi cha asili zote za uombezi kama isemavyo Qur`an Tukufu, "Na lau wanalikujia walipojidhulumu nafsi zao wakaomba msamaha, bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu Mwenye kupokea toba, Mwenye Rehema." (4:65). Kadhalika tunasoma katika Qur`an Tukufu, "Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe kwayo na kuwatakasana na uwaombe; hakika kuomba kwako ni utulivu kwao" (Sura 9:103).



Aya hizi na nyinginezo nyingi kama hizi zinashuhudia kwamba Nabii Muhammad s.a.w; alikuwa mwombezi kwa walimwengu na kwamba uombezi wake utawaongoza wale walio wanyonge nao watapata heshima.

Mwenyezi Mungu amewabariki sehemu ya cheo cha uombezi wafuasi watii wa Nabii Muhammad s.a.w. Kwa mfano Masihi Aliyehidiwa a.s. Hadhrat Ahmad wa Qadian, wakati wa uhai wake alijaaliwa uwezo wa kuwaombea watu, wengine waliokaribia kufa, lakini kwa dua zake wameweza kuishi hata sasa (wakati mtunzi alipokuwa hai) kama thibitisho dhahiri la kukubaliwa kwa uombezi wa Masihi Aliyehidiwa a.s. na Mwenyezi Mungu. Baada ya Masihi Aliyehidiwa a.s. imeendelea kushuhudia kutimizwa kwa uombezi wa Makhalfi wake watukufu. Wamebarikiwa wale wote wenye kuyakubali haya na kufuata njia iliyonyooka iongozayo kwenye uzima wa milele.

Ewe Mwenyezi Mungu mwenye uwezo wote! Ziondoe kufuru za kidunia na uwaongoze viumbe wako katika njia yenye kuwaepusha dhambi! Uwafunue macho yao waweze kuiona njia ya ukweli ili waweze kuifikia chemchem ya elimu ya yakini wapate kunywa hapo maridhawa! Amin.

**JESUS' ATONEMENT**  
**(Swahili Translation)**

This book was first written in English by Dr. Mufti Muhammad Sadiq r.a., the first Ahmadiyya Missionary in America.

The book discusses shortly but precisely on the following topics:

- The need for Atonement
- Disapproval of Atonement theory
- Historical facts about Atonment
- Why we are rejecting Atonment
- The origin of Atonment
- How to get rid of Sins

We hope that the book will benefit those who will read it thoughtful